Somo

la

Mwanzo

1:1 – 12:8

Na
David Jett

Hatua Nne Za Mwanzo Wa Maandiko ...

1. <u>UUMBAJI</u> - <u>MWANZO</u> wa Mwanadamu

2. <u>UHARIBIFU</u> – <u>ANGUKO</u> la Mwanadamu

3. <u>UKOMBOZI</u> - <u>KUKOMBOLEWA</u> kwa mwanadamu

4. <u>UFUFUO</u> – <u>UREJESHO</u> wa Mwanadamu

Mwanzo na hatima ya Biblia

Sura mbili za kwanza katika biblia zinazungumza juu ya UUMBAJI.

Mwanzo 1:1 (ESV)

Mwanzo 2:4 (ESV)

Sura mbili za mwisho katika Biblia zinazungumza juu ya UFUFUO.

Ufunuo 21:1 (ESV)
[1] Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpoya, kwa kuwa mbingu za kwanza na nchi za kwanza zimepita

Uumbaji – Mwanzo wa Mwanadamu

Mwanzo 1:1 – 2:25

1. Uumbaji <u>Unatokana</u> na Mungu.

Mwanzo 1:1 (ESV)
[1] Hapo Mwanzo, Mungu aliziumba mbingu na nchi.

2. Uumbaji <u>UNAHUSISHA</u> Utatu.

A. Mungu, Baba - <u>Mapenzi</u> ya Mungu.

B. Mungu, Roho - <u>UPEPO</u> wa Mungu.

Mwanzo 1:2 (ESV)
[2] Nayo nchi ilikuwa ukiwa tena utupu nagiza lilikuwanjuu ya uso wa vilindi vya maji.

C. Mungu, Mwana – <u>Neno</u> la Mungu.

Mwanzo 1:3 (ESV)
[3] Na Mungu akasema ...

Yohana 1:1–2 (ESV)
[1] Hapo mwanzo kulkikuwa na Neno naye Neno alikuwa kwa Mungu na Naye Neno alikuwa ni Mungu. [2] Huyo Mwanzo alikuwako kwa Mungu.

3. Uumbaji hupata <u>MAANA</u> kupitia kwa Mungu

Mwanzo 1:2 (ESV)
[2] Nayo nchi ilikuwa ukiwa tena utupu na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji.

Siku Sita Za Uumbaji

Kufanya	***Kujaza***
Siku ya 1 – Nuru	***Siku ya 4 – Nuru***
Siku ya 2 – Hewa na maji	***Siku ya 5 – Ndege & Samaki***
Siku ya 3 – Nchi & Mimea	***Siku ya 6 – Wanyama & Mwanadamu***

4. Uumbaji umetawaliwa na <u>MWANADAMU</u> chini ya Mungu

Mwanzo 1:26–28 (ESV)
[26] Mungu akasema, "na tumfanye mtu kwa mfano wetu kwa sura yetu wakatawale samaki wa baharini na ndege wa angani na wanyama na nchi yote pia na kila chenye kutambaa kitambaacho chini ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake kwa mfano wa Mungu alimuumba mwanamume na Mwanamke aliwaumba. Mungu akawabariki Mungu akawaambia zaeni mkaongezeke mkaijaze nchi na kuitiisha; mkawatawale samaki wa baharinina ndege wa angani na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi."

A. Mwanadamu ameumwa kwa ajili ya <u>MAHUSIANO</u> na Mungu

B. Mwanadamu ameumbwa ili <u>ATAWALE</u> chini ya Mungu

Mwanzo 2:25 (ESV)
[25] Na walikuwa uchi wote wawili Adamu na mkewe wala hawakuona haya.

Upotofu – Anguko la Mwanadamu

Mwanzo 3:1-24

Katika sura hii moja tunaambia KWELI NNE ZA KIROHO kuhusiana na anguko la Mwanadamu

1 – JARIBU

Msingi → Adamu na Eva hawakuumbwa na ASILI ya kutenda dhambi bali waliumbwa na UWEZEKANO wa kutenda dhambi

2 – DHAMBI

Dhambi → TATHIMINI ya kuishi maisha yetu pasipo KUMTEGEMEA

Mwanzo 3:6 (ESV)
6 Mwanamke alipoona ya kwamba mti ule wafaa kwa chakula wapendeza macho nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa basi alitwaa katika matundayake akala akampa na mmewe naye akala.

3 – HUKUMU

A. KUSHTAKIWA DHAMIRI YA NDANI

Mwanzo 3:7–8 (ESV)
7 Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi wakashona majani ya mti wakajifanyia nguo.. 8 kisha wakaisikia Sauti ya Bwana Mungu akitembea biustanini wakati wa ua kupunga Adamu na mkewe wakajificha Mungu asiwaone.

B. HUKUMU

Mwanzo 3:9–13 (ESV)

[9] Bwana Mungu akamwita Adamu akamwambia, "Uko wapi?" akasema nalisikia sauti yako bustanini nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi nikajificha. Akasema ni nani aliyekwambia ya kuwa wewe u uchi? Je umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usile? Adamu akasema huyo mwanamke uliye nipa awe pampja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. Bwana Mungu akamwambia mwanamke nini ulilolifanya? Mwanamke akasema nyoka alinidanganya, nikala."

Wagalatia 6:7–8 (ESV)

[7] Msidanganyike Mungu hadhihakiwi kwakuwa chochote apandacho mtu ndicho atakachovuna.. [8] maana yeye apandaye katika mwili wake katika mwili wake atavuna uharibifu bali yeye apandaye kwa Roho katika Roho atavuna uzima wa milele.

- ***Mara zote tunavuna KILE tunachopanda, BAADA ya kupanda na hata ZAIDI YA vile tunavyopanda***

C. UTENGANO

Mwanzo 3:23–24 (ESV)

[23] Kwa hiyo Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya edeni ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa. [24] Basi akamfukuza huyo mtu akaweka Makerubi upande wa mashariki wa bustani ya edeni na upanga wa moto uliogeuka huko na huko.

Isaya 59:2 (ESV)

[2] lakini maovu yenu yamewafarakanisha ninyi na Mungu wenu na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone hata hatakki kusikia.

Ukombozi – kuokolewa kwa Mwanadamu

A. <u>AHADI</u> ya kuja kwa Mkombozi

Mwanzo 3:15 (ESV)
[15] nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke na kati ya uzao wako na uzao wake huo utakuponda kichwa wewe utamponda kisigino."

Wagalatia 4:4–5 (ESV)
[4] Hata ulipowadia utimilifu wa wakati Mungu alimtuma mwanae ambaye amezaliwa na mwanamke amezaliwa chini ya sheria. Kusudi awakomboe hao walio chini ya sheria ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana..

Yesu ni Ahadi ya Mungu ya kutukomboa!

1 Yohana 3:8 (ESV)
[8] Atendaye dhambi ni waibilisi kwakuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili mwana wa Mungu alidhihirishwa. Ili azivunje kazi za Ibilisi.

B. <u>TASWIRA</u> ya Gharama za ukombozi

Mwanzo 3:20–21 (ESV)
[20] Adamu akamwita mkewe jina lake hawa kwakuwa yeye ndiye aliye mama yao wote walio hai. Bwana Mungu akawafanyia Adamu na Mkewe mavazi ya ngozi akawavika.

C. ULINZI kwa ajili ya Ukombozi kamili The <u>PROTECTION</u> for certain Redemption

Mwanzo 3:22–24 (ESV)
[22] Bwana Mungu akasema basi mtu huyu amekuwa kama mmoja wetu kwa kujua mema mna mabaya na sasa asije akanyoosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima akala akaishi milele—" [23] Kwa hiyo Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa. Basi akamfukuza mtu huyo akaweka makerubi upande wa mashariki wa bustani ya edeni na upanga wa moto uliogeuka huko na huko kuilinda njia ya mti wa uzima.

Wana Watatu wa Adamu

Mwanzo 4 - 5

1. KAINi – Mwana ALIYELANIWA

Mwanzo 4:1–2 (ESV)
[1] Adamu akamjua hawa mkewe naye akapata Mimba akamzaa kaini. Akasema nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana. Akaongeza akamzaa ndugu yake habili habili alikuwa mchunga kondoo na kaini alikuwa mkulima wa ardhi.

Jlna "Kaini" linamaanisha "Umiliki"

Mwanzo 4:3–5 (ESV)
[3] Ikawa hatimaye kaini akaleta mazao ya ardhi sadaka kwa Bwana. Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. Bwana akamtakabali habili na sadaka yake . Bali kaini hakumtakabali wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana uso wake ukakunjamana.

Mwanzo 4:6–7 (ESV)
[6] Bwana akamwambia Kaini kwa nini unaghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana? Kama ukitenda vyema hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko. Inakuotea mlangoni nayo inakutamani wewe walakini yakupasa uishinde."

Yakobo 1:14–15 (ESV)
[14] lakini kila mmoja hujaribiwa na tama yake mwenyewehuku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikisha kuchukua mimba huzaa dhambi na ile dhambi ikisha kukomaa huzaa mauti.

A. LAANA – maisha bila MUNGU

Mwanzo 4:11–12 (ESV)
[11] Basi sasa umelaaniwa wewe katika Ardhi iliyofumbua kinywa cghake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako. Utakapoilima Ardhi haitakupa mazao yake utakuwa mtoro na mtu asiyekuwa na kikao duniani."

Mwanzo 4:16 (ESV)
[16] Kaini akatoka mbele za uso wa Bwana akakaa katika nchi ya Nodi mbele ya Nodi.

B. akuzungukazunguka – Maisha Bila MAANA

Mwanzo 4:17 (ESV)
[17] kaini akamjua mkewe naye akapata mimba akamzaa henoko akajenga mji akauita Henoko kwa jina la mwanae.

Mwanzo 4:19 (ESV)
[19] Lameki akajitwalia wake wawili jina la wa kwanza ni Ada na jina la wa pili ni Sila.

Mwanzo 4:20–22 (ESV)
[20] Ada akamzaa Yabali huyo ndiye baba yao akaao katika hema na kufuga wanyama. Na jina la nduguye aliitwa Yubali huyo ndiye baba yao wapigao kinubi na filimbi. Mfua kila chombo cha kukatia cha shaba na cha chuma. Na umbu lake Tubal-kaini alikuwa Naama.

C. <u>VURUGU</u> – maisha bila <u>AMANI</u>

Mwanzo 4:23–24 (ESV)

23 3

Lameki akawaambia wake zake, "Ada na Sila nisikilizeni mimi, Wake wa Lameki sikieni maneno yangu. Nimemwua mtu kwa kunijeruhi, kijana mdogo kwa kuniumiza

24Kama Kaini atalipizwa kisasi mara saba, basi Lameki itakuwa mara sabini na saba.

Yuda 1 (ESV)

11 Ole wao! Kwa kuwa wanaifuata njia y Kaini, wamekimbilia faida katika kosa la Baalamu na kuangamia katika uasi wa Kora*.*

2. <u>HABILI</u> – Mwana wa <u>HAKI</u>

Jina "habili" linamaanisha "Tupu"

Muhubiri 1:2 (ESV)

2 "Ubatili mtupu! Ubatili mtupu!" Mhubiri anasema. "Ubatili mtupu! Kila kitu ni ubatili."

1 Yohana 3:12 (ESV)

12 Msiwe kama Kaini aliyekuwa wa yule mwovu akamwua ndugu yake. Basi kwa nini alimwua? Ni kwa sababu matendo yake Kaini yalikuwa mabaya na ya ndugu yake yalikuwa ya haki

.

Waebrania 11:4 (ESV)

4 Kwa imani Abeli alimtolea Mungu dhabihu bora zaidi kuliko Kaini.Kwa imani alishuhudiwa kuwa mwenye haki,Mungu mwenyewe akazishuhudia sadaka zake. Kwa imani bado ananena ingawa amekufa.

3. <u>SETH</u> – Mwana <u>ALIYEBARIKIWA</u>

Mwanzo 4:25 (ESV)

25 Adamu akakutana kimwili na mke wake tena, akamzaa mwana akamwita Seti, akisema, "Mungu amenijalia mwana mwingine badala ya Abeli, kwa kuwa Kaini alimwua.

Jina "Seth" linamaanisha "Aliyechaguliwa"

Mwanzo 4:26 (ESV)

26 Pia Seti akamzaa mwana akamwita Enoshi. Wakati huo watu wakaanza kuliitia jina la BWANA.

Nuhu na Gharika

Mwanzo 6 – 9:17

1. UHARIBIFU wa Mwanadamu

Mwanzo 6:1–5 (ESV)

1 Watu walipoanza kuongezeka idadi katika uso wa dunia na watoto wa kike wakazaliwa kwao,
2wana wa Mungu wakawaona kuwa hao binti za wanadamu walikuwa wazuri wa sura, wakaoa ye yote miongoni mwao waliyemchagua.
3Ndipo BWANA akasema, "Roho yangu haitakaa ndani ya mwanadamu milele, kwa kuwa yeye ni wa kufa, siku zake zitakuwa miaka 120.''
4Wanefili walikuwako duniani siku hizo, pia na baadaye, hao walizaliwa na binti za watu wakati wana wa Mungu walipoingia kwao na kuzaa nao. Wanefili walikuwa mashujaa na watu waliojulikana wa zamani hizo.
5BWANA akaona jinsi ambavyo uovu wa mwanadamu umekuwa mkubwa duniani na ya kuwa kila mwelekeo wa mawazo ya moyo wake wakati wote ulikuwa mbaya tu.

2. Dhambi ya Mwanadamu huleta <u>HUKUMU</u>

Mwanzo 6:6–7 (ESV)

6 BWANA akasikitika kwamba alimwumba mwanadamu duniani, moyo wa Mungu ukajaa masikitiko.
7Kwa hiyo BWANA akasema, "Nitamfutilia mbali mwanadamu niyemwumba kutoka kwenye uso wa dunia, wanadamu na wanyama, pamoja na viumbe vitambaavyo na ndege wa angani. Kwa maana nasikitika kwa kuwaumba.'

Mwanzo 6:11–13 (ESV)

11 Wakati huu dunia ilikuwa imejaa uharibifu na jeuri machoni pa Mungu.
12Mungu akaona jinsi dunia ilivyoharibika, kwa maana watu wote duniani walikuwa wameharibu njia zao.
13Kwa hiyo Mungu akamwambia Nuhu Nitawaangamiza watu wote, kwa kuwa dunia imejaa jeuri kwa sababu yao. Hakika mimi nitaangamiza watu pamoja na dunia.

3. Mungu huonesha <u>HURUMA</u> kwa mwanadamu kupitia Nuhu

Mwanzo 6:3 (ESV)

3 Ndipo BWANA akasema, "Roho yangu haitakaa ndani ya mwanadamu milele, kwa kuwa yeye ni wa kufa, siku zake zitakuwa miaka 120."

Mwanzo 6:8–9 (ESV)

8 Lakini Noa akapata kibali machoni pa BWANA.
9Hivi ndivyo vizazi vya Noa. Noa alikuwa mtu wa haki, asiye na lawama miongoni mwa watu wa wakati wake, tena alitembea na Mungu.

Mwanzo 6:17–18 (ESV)

17 Nitaleta gharika ya maji juu ya nchi ili kuharibu uhai wote chini ya mbingu, kila kiumbe chenye pumzi ya uhai ndani yake. Kila kitu juu ya nchi kitaangamia.
18Lakini Mimi nitaweka agano langu na wewe, nawe utaingia ndani ya Safina, wewe pamoja na mke wako, wanao na wake zao.

Mwanzo 7:1 (ESV)

1 Ndipo BWANA akamwambia Noa, "Ingia katika safina wewe na jamaa yako yote, kwa sababu katika kizazi hiki nimeona ya kuwa wewe ni mwenye haki.

4. Mungu <u>AISAFISHA</u> dunia kwa gharika

Mwanzo 7:11–12 (ESV)

11 Katikasiku ya kumi na saba ya mwezi wa pili mwaka wa 600 wa kuishi kwake Noa, siku hiyo ndipo chemchemi zote hata zilizo chini sana ya ardhi zilibubujika kwa nguvu, na malango ya mafuriko ya mbinguni yakafunguliwa.
12Mvua ikanyesha juu ya nchi siku arobaini mchana na usiku.

Wana Watatu Wa Nuhu

Mwanzo 9:18 – 10:32

Mwanzo 6:10 (ESV)

10 Nuhu alikuwa na wana watatu: Shemu, Hamu na Yafethi.

Mwanzo 9:18–29 (ESV)

18 Wana wa Noa waliotoka ndani ya safina ni: Shemu, Hamu na Yafethi. (Hamu ndiye aliyekuwa baba wa Kanaani.)
19Hawa ndio waliokuwa wana watatu wa Noa, kutokana nao watu walienea katika dunia.
20Noa akawa mkulima, akawa mtu wa kwanza kupanda mizabibu.
21Alipokunywa huo mvinyo wake akalewa na akalala uchi kwenye hema lake.
22Hamu, baba wa Kanaani, akauona uchi wa baba yake na kuwaeleza ndugu zake wawili waliokuwa nje.
23Lakini Shemu na Yafethi wakachukua nguo wakaitanda mabegani mwao wote wawili, kisha wakaenda kinyumenyume, wakaufunika uchi wa baba yao. Nyuso zao zilielekea upande mwingine ili wasiuone uchi wa baba yao.
24Noa alipolevuka kutoka kwenye mvinyo wake na kujua lile ambalo mwanae mdogo kuliko wote alilokuwa amemtendea,
25akasema, "Alaaniwe Kanaani! atakuwa mtumwa wa chini sana kuliko watumwa wote kwa ndugu zake."
26Pia akasema Abarikiwe BWANA Mungu wa Shemu! Kanaani na awe mtumwa wa Shemu.
27Mungu na apanue mipaka ya Yafethi, Yafethi na aishi katika mahema ya Shemu, Kanaani na awe mtumwa wake."
28Baada ya gharika Noa aliishi miaka 350.
29Noa alikuwa na jumla ya miaka 950, ndipo akafa.

1. Wana Wa Yafeti

Mwanzo 10:1–2 (ESV)

1 Hawa ndio wazao wa Noa: Shemu, Hamu na Yafethi, ambao walizaa wana baada ya gharika
. 2 Wana wa Yafethi walikuwa: Gomeri, Magogu, Madai, Yavani, Tubali, Mesheki na Tirasi.

2. Wana Wa Hamu

Mwanzo 10:6 (ESV)

6 Wana wa Hamu walikuwa: Kushi, Misri, Puti na Kanaani.

3. Wana Wa Shemu

Mwanzo 10:22 (ESV)

22 Wana wa Shemu walikuwa: Elamu, Ashuru, Arfaksadi, Ludi na Aramu.

Europe
ASIA
Africa
Magog
Gomer
Meshech
Tiras
Caspian Sea
Black Sea
Table of Nations
Genesis 10
Tubal
Javan
Lud
Asshur
Madai
Mediterranean Sea
Canaan
Aram
Arphaxad
Elam
Cush
Lud
Phut
Hindustan
Arabia
Indian Ocean
Mizarim
Cush
Bible History Online

Mnara wa Babeli

Mwanzo 11:1-9

1. Watu wote ni <u>JAMII</u> moja

Mwanzo 11:1–2 (ESV)

[1] Wakati huo dunia yote ilikuwa na lugha moja na msemo mmoja.
[2]Watu walipoelekea upande wa mashariki, wakafika kwenye tambarare katika nchi ya Shinari nao wakaishi huko
.

2. Watu wote <u>WANAHITAJI</u> moja

Mwanzo 11:3–4 (ESV)

[3] Wakasemezana wao kwa wao, "Njoni, tufyatue matofali na tuyachome vizuri kwa moto.'' Walitumia matofali badala ya mawe, na lami kwa ajili ya kulinganishia hayo matofali.
[4]Ndipo wakasema, "Njoni, tujijengee mji wenye mnara ambao utafika hadi mbinguni, ili tujipatie jina tusije tukatawanyika usoni pa dunia yote.''

3. Watu wote WANATUMAINI moja

Mwanzo 11:5–9 (ESV)

[5] Lakini BWANA akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wanaujenga wanadamu.
[6]Kama taifa moja wanaozungumza lugha moja wameanza kufanya hili, basi hakuna lo lote watakalopanga kufanya ambalo halitawezekana kwao.
[7]Njoni, tushuke tuvuruge lugha yao ili wasielewane wao kwa wao."
[8]Hivyo BWANA akawatawanya kutoka mahali pale kwenda katika dunia yote, nao wakaacha kuujenga huo mji.
[9]Ndiyo maana pakaitwa Babeli, kwa sababu hapo ndipo BWANA alipoivuruga lugha ya dunia nzima. Kutoka hapo BWANA akawatawanya katika uso wa dunia yote.
.

Kuitwa Kwa Ibrahimu

Mwanzo 11:10 – 12:9

Mwanzo 12:1–3 (ESV)

1 BWANA akawa amemwambia Abramu, “Ondoka katika nchi yako, waache watu wako na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha.
2“Mimi nitakufanya taifa kubwa na nitakubariki, Nitalikuza jina lako, nawe utakuwa baraka.
3Nitawabariki wale wanaokubariki, yeyote akulaaniye nitamlaani na kupitia kwako mataifa yote duniani yatabarikiwa.

1. Abrahamu aliitwa ili <u>ATENGWE</u> kutoka katika watu wote

Mwanzo 12:4–6 (ESV)

4 Hivyo Abramu akaondoka kama BWANA alivyokuwa amemwambia, naye Loti akaondoka naye. Wakati Abramu alipoitwa aondoke Harani, alikuwa na miaka sabini na mitano.
5Abramu akamchukua Sarai mkewe pamoja na Loti mwana wa ndugu yake, mali zote walizokuwa nazo pamoja na watu aliokuwa amewapata huko Harani, wakasafiri mpaka nchi ya Kanaani, wakafika huko.
6Abramu akasafiri katika nchi hiyo akafika huko Shekemu, mahali penye mti wa mwaloni ulioko More. Wakati huo Wakanaani walikuwa wanaishi katika nchi hiyo.

Matendo 7:2–3 (ESV)

2 Stefano akajibu, “Ndugu zangu na baba
zangu, nisikilizeni! Mungu wa utukufu alimtokea
baba yetu Abrahamu, alipokuwa bado yuko Mesopotamia, kabla hajaishi Harani,
3akamwambia, ‘Ondoka katika nchi yako na kutoka kwa jamii yako uende katika nchi nitakayokuonyesha

1 Yohana 2:15–17 (ESV)

15 Msiupende ulimwengu wala mambo yaliyoko ulimwenguni. Kama mtu ye yote akiupenda ulimwengu,kumpenda Baba hakumo ndani yake.
16Kwa maana kila kitu kilichomo ulimwenguni, yaani, tamaa ya mwili, tamaa ya macho na kiburi cha uzima, havitokani na Baba bali hutokana na ulimwengu.
17Nao ulimwengu unapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu milele.

2. Abrahamu aliitwa ili awe <u>MKUU</u> kati ya watu wote

Mwanzo 12:2 (ESV)

2 Mimi nitakufanya taifa kubwa na nitakubariki, Nitalikuza jina lako, nawe utakuwa baraka
.

Mwanzo 12:7 (ESV)

7 BWANA akamtokea Abramu akamwambia, “Nitawapa uzao wako nchi hii.’’ Hivyo hapa Abramu akamjengea BWANA madhabahu, ambaye alikuwa amemtokea.

3. Abrahamu aliitwa ili awe ni BARAKA kwa watu wote

Mwanzo 12:3 (ESV)

3 Nitawabariki wale wanaokubariki, yeyote akulaaniye nitamlaani na kupitia kwako mataifa yote duniani yatabarikiwa.”

Mwanzo 12:8 (ESV)

[8] Kutoka huko Abramu akasafiri kuelekea kwenye vilima mashariki ya Betheli, naye akapiga hema huko, Betheli ikiwa upande wa magharibi na Ai upande wamashariki. Huko alimjengea BWANA madhabahu na akaliitia jina la BWANA